**Learning by Ear – Girls' Rights**

**Episode 05**

**Title: Child Labour - A story of Girls' Rights**

**Author: Njoki C. Muhoho**

**Editors: Andrea Schmidt, Katrin Ogunsade**

**Proofreading: Michael Lawton**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

**Characters:**

**SCENE 1 SCHOOL PLAYING FIELDS**

Narrator - 30s Male
Ciro - 14 Female
Cheptoo - 15 Female
Fatuma - 14 Female
Kid - About 10

**SCENE 2 - SCHOOL PLAYING FIELDS**

Ciro - 14 Female
Cheptoo - 15 Female
Narrator - 30s Male

**SCENE 3 - FOOTPATH TO FATUMA'S PARENT'S HOME**

Ciro - 14 Female
Cheptoo - 15 Female
Fatuma - 14 Female
Narrator - 30s Male

**SCENE 4 - FATUMA'S PARENTS' HOMESTEAD**

Elder Jacob - 60s Male
Teacher Mona - 35 Female
Ciro - 14 Female
Cheptoo - 15 Female
Fatuma - 14 Female

Janet-Social Worker - 30s Female
Narrator - 30s Male

**01. INTRO**

**02. MUSIC: THEME MUSIC**

03. **NARRATOR** Hujambo na karibu kwa makala ya tano kwenye mfululizo wa vipindi vya Noa Bongo Jenga Maisha yako kuhusu **'Haki za Wasichana'** Katika kipindi kilicho tangulia Ciro ampoteza Babake. Na Babake mdogo Babu,atangaza mipango ya kurithi mali ya Mama Ciro. Marafiki wa Ciro, Fatuma na Cheptoo pamoja na Abdi,binamuye Ciro, wanafahamu kwamba Wasichana pia wanahaki ya kurithi mali.
Katika kipindi cha leo wanafunzi hawa wanashangazwa na suala na ajira kwa watoto.Tuungane nao wanapo jadilia hoja hili ya '**Ajira kwa Watoto**'.

**SCENE 1: SCHOOL PLAYING FIELD**

**04. SFX: PLAY FIELD NOISES**

**05. SFX: CHEPTOO CHEWING NUTS (studio)**

06. **CIRO** (ADMONISHING) Cheptoo, tafadjhali funga mdomo wako unapotafuna.

07. **CHEPTOO** (FULL MOUTH) Wewe hujui, jinsi njugu hizi zilivyo tamu. Onja kidogo.

08. **FATUMA** Lakini silazima utafune mdomo ukiwa wazi ndio kupata utamu zaidi.

PAUSE

09. **CIRO** (SHOUTING) Chunga,. Chunga.. chunga Nzi, Nzi huyo Fatuma… angalia unatafuna nzi ….

**10. <u>SFX: CHEPTOO CHOKING AND SPLUTTERING</u>**

**11. <u>SFX: LAUGHTER – CIRO AND FATUMA</u>**

12. **CIRO** (LAUGHING) Umemtafuna… umemtafuna inzi …!

13. **CHEPTOO** (SPLUTTERING) Nini,..nini…ohh… ooh hapana..yuk…yuk…Nafikiri sasa nitakuwa mgonjwa!

14. **FATUMA** (LAUGHING) Nzi mkubwa ,mkuuuubwa.

**15. <u>SFX: MORE SPLUTTERING. CHOKING AND COUGHING</u>**

16. **CHEPTOO** Ooh hapana… yuk… yuk… yuk….

17. **CIRO** (LAUGHING) hahahaha…Nilikuwa nakutania tu!.

18. **CHEPTOO** Yaani .. kwa hiyo si nzi.

**19. SFX: FATUMA & CIRO. LAUGH HYSTERICALLY.**

| | | |
|---|---|---|
| 20. | **CHEPTOO** | Sasa angalia ulivyofanya . Hizi zilikuwa njugu zangu za mwisho. |
| 21. | **CIRO** | Sawa, Cheptoo, nitakununulia nyingine, wako wapi hawa watoto wakuuza njugu? Nyinyi… nyinyi watoto wauza njugu…njooni hapa. |

**22. <u>SFX: FOOT STEPS APPROACH</u>**

| | | |
|---|---|---|
| 23. | **CIRO** | Tuuzieni njugu nyingine. Pesa hizi!. |

**24. <u>SFX: COINS RATTLE</u>**

| | | |
|---|---|---|
| 25. | **FATUMA** | Kwanini munauza Njugu badala a kwenda shule? |
| 26. | **KID** | Sisi hatwendi shule. |
| 27. | **CIRO** | Kwanini? |
| 28. | **KID** | Tunataka kufanya biashara hii ya kuuza njugu ili tupate pesa.Tumetumwa na wazazi wetu kuuza njugu. Na nilazima turudi nyumbani na pesa. |
| 29. | **FATUMA** | Lakini ni lazima mwende shule? |

**30. <u>SFX: SCHOOL BELL</u>**

| | | |
|---|---|---|
| 31. | **CHEPTOO** | Watoto niuzieni nyingine!. |

**SCENE 2 SCHOOL PLAYING FIELDS**

32. **NARRATOR** **The other day, Cheptoo and Ciro meet at school. But where is Fatuma?**

33. **SFX: BELL RINGS. DOORS OPEN AND SLAM**

34. **SFX: END OF SCHOOL DAY NOISES STUDENTS MUTED NOISES.**

35. **CHEPTOO** (SHOUTING) Ciro! Ciro!Njoo hapa.

36. **CIRO** (SHOUTING) Cheptoo, subiri kidogo.

37. **CHEPTOO** Umemuona Futuma? Nimemtafuta kila mahali.

38. **CIRO** Labda amechelewa tena darasani.

39. **CHEPTOO** Nimeenda kumtafuta nikaambiwa hakufika shuleni leo.

40. **CIRO** Ooh kwanini, kwani kumetokea nini tena?.

41. **CHEPTOO** Twende upesi nyumbani kwao tukamwangalie, labda ana matatizo.

42. **NARRATOR** Ciro, Cheptoo na Fatuma ni wanafunzi katika madarasa tofauti, lakini hukutana kila baada ya masomo. Fatuma amekosekana tena...

Ciro na Cheptoo wanaamua kwenda kumtembelea nyumbani kwao baada ya masomo. Kwani nyumba yao haiko mbali sana na shule.

**SCENE 3: FOOT PATH TO FATUMA PARENTS' HOME**

**43. SFX: TWO SETS OF FOOTWORK ON PATH**

**44. SFX: STOMACH RUMBLES**

45. **CIRO** Cheptoo!! Usifanye hivyo,Mtu atadhani unakikundi cha wacheza ngoma tumboni.

46. **CHEPTOO** Si kosa langu, ni zile njugu nilizokula! Zanisumbua…zimenijaza tumbo.

47. **CIRO** Basi usizile tena.Umekula nyingi sana.

48. **CHEPTOO** Lakini ni biashara nzuri kwa watoto wale!..Tazama.. nadhani yule ni...ni… Fatuma.

**49. SFX: RUNNING FEET.**

50. **CIRO/CHEPTOO** Fatuma! Fatuma…!

| | | |
|---|---|---|
| 51. | **FATUMA** | (VERY TIRED) Naaaam. |

**52. <u>SOUND: OUT OF BREATH AND PANTING</u>**

| | | |
|---|---|---|
| 53. | **CHEPTOO** | Una matatizo gani wewe msichana? Kwanini hukwenda shule leo? Kwanini unabeba mzigo mkubwa hivi? |
| 54. | **CIRO** | Fatuma, waonekana umechoka sana…tena mchafu...! |
| 55. | **FATUMA** | Nimekuwa nikifanya kazi mchana kutwa… nimechoka sana… |
| 56. | **CHEPTOO** | (FIRMLY) Subiri wewe msichana… nani amekutuma ufanye kazi… tazama ulivyomchafua . |
| 57. | **CIRO** | Cheptoo, kwani huoni Fatu anavyoteseka..! Fatu.. waonekana uko na njaa sana. |
| 58. | **CHEPTOO** | Karibu Njugu!. |
| 59. | **CIRO** | Usichukue,utaanza kutoa pumzi kama gari moshi. |
| 60. | **CHEPTOO** | Kwani humuoni huyu msichana ana njaa. |
| 61. | **FATUMA** | Niacheni niende tafadhali nachoka, hamuoni huu mzigo ni mzito. |

62. **CIRO** Cheptoo… Tumsaidie mzigo. Tumsaidie!

63. **CHEPTOO** Mimi ni bebe mzigo huu?…. Fatuma anataka kubeba, mwache aubebe.. .! Mimi sitabeba mzigo mzito na mahfu hivi..! kwani umebeba nini? Mawe??

64. **FATUMA** Nisaidieni.,.!

65. **<u>SFX: HEAVING AND SIGHING (studio)</u>**

66. **<u>SFX: LOAD LANDS ON GROUND WITH THUD</u>.**

67. **FATUMA** phew….(SIGH),Afadhali sasa..!

68. **CIRO** Njooni tuketi pale. Fatuma anahitaji kupumzika, na kisha atueleze haya yote.

69. **FATUMA** Ni wazazi wangu!. Wanasema hatuna pesa za kutosha kununua chakula na kulipa karo yangu.Wananiambia mimi nimekuwa msichana mkubwa, lazima nitafute kibarua nifanye tupate pesa za kununua chakula cha familia nzima.

70. **CHEPTOO** Na shule je?

71. **CIRO** Eeehhh..shule na sisi marafiki wako je?

| | | |
|---|---|---|
| 72. | **FATUMA** | Sasa kuna maana gani ya kwenda shule kama hakuna chakula nyumbani, na pesa za kulipa karo au kununua sare za shule?Napasa kuwatafutia chakula kaka na dada zangu!. |
| 73. | **CHEPTOO** | Lakini hilo ni jukumu la wazazi!.Wanapasa kukupa chakula na kukuelimisha. |
| 74. | **CIRO** | Fatuma, wewe si wazazi wao? |
| 75. | **FATUMA** | Hebu sema hivyo kwa wazazi wangu, utajuta!. |
| | | SILENCE |
| 76. | **CIRO** | Sasa tufanye nini? |
| 77. | **CHEPTOO** | Mmmmm …Nina wazo. Tumsaide Fatuma kufika nyumbani .Kisha kesho tufanye mpango na mwalimu Mona na afisa Janet, tutaitisha kikao cha bunge la wasichana'. |
| 78. | **FATUMA** | Hakuna haja? Mutajadiliana miaka na miaka lakini wazazi wangu hawatasikia la muadhini wala la mteka maji. |

| | | |
|---|---|---|
| 79. | **CIRO** | (EXCITED) Nidhani nina wazo bora, tuitishe kikao cha bunge la wasichana nyumbani kwenu. |
| 80. | **FATUMA** | Vipi? Vipi utaweza kufanya hivyo? |
| 81. | **CHEPTOO** | Niachie mimi!. |
| 82. | **NARRATOR** | Wasichana hao sasa wanakumba na changamoto zaidi.Jinsi ya kuwashawishi wazazi kuhusu athari za ajira kwa watoto. Sasa wanafahamu kuwa vikao vya bunge la wasichana mara nyingi havitoi ufumbuzi wa matatizo yao.Wanataka kuzihusisha pande zote husika,moja kwa moja katika kutafuta sulughisho la tatizo hili. |

**SCENE 4: FATUMA'S PARENTS' HOMESTEAD**

**83. SFX; FARM NOISES**

| | | |
|---|---|---|
| 84. | **ELDER JACOB** | Mwalimu Mona na Afisa Janet…! Japo mwakaribishwa katika nyumba hii, nashangaa kwanini mumenitembelea saa na wakati kama huu. Fatuma haolewi tena sasa! na tulikubaliana hivyo...! Sasa mmekuja kutafuta nini tena nyumbani kwangu? |

| | | |
|---|---|---|
| 85. | **TEACHER MONA** | Mzee Jacob, tuko hapa kwasababu ya binti yako Fatuma.Tumeandamana na baadhi ya wasichana kutoka shuleni. Wasichana msalimieni Mzee Jacob. |
| 86. | **CIRO/CHEPTOO** | Habari za mchana Mzee Jacob. |
| 87. | **ELDER JACOB** | Ni njema. Nini kinachomleta hapa? |
| 88. | **CIRO** | Mimi ni Ciro, rafiki mkubwa wa Fatuma. |
| 89. | **CHEPTOO** | Mzee Jacob, naitwa Cheptoo, na tunasikitika sana kuhusu hali aliyomo mwenzetu Fatuma.Leo hakufika shuleni na ndilo jambo linalotuleta hapa. Tulizungumzie na pia kutoa heshima zetu kwa wazazi wake. |
| 90. | **ELDER JACOB** | Ohh vizuri sana …nyinyi ni marafiki wazuri. |
| 91. | **CHEPTOO** | Ndio…sisi ni marafiki wakubwa sana Mzee Jacob.Ndio sababu tunataka kukuomba utupe muda wa kuzungumza nawe kuhusu hali ya Fatuma. |

| | | |
|---|---|---|
| 92. | **ELDER JACOB** | Hali ya Fatuma?.Yeye anafanya kazi ili kukimu mahitaji yake maishani,na kufanya hivyo sio kifo?Wacheni ni waeleze nyinyi wasichana. Watoto wanapasa kufanya kazi kusaidia Familia zao. |
| 93. | **CHEPTOO** | Ndio, lakini mimi natoa hoja hii, kwamba Watoto na hawapasi kufanyishwa kazi, na tabia hii lazima ikomeshwe. |
| 94. | **ELDER JACOB** | Unataka kutoa hoja?? |
| 95. | **JANET** | Mzee Jacob,nadhani unanifahamu vyema, naitwa Janet afisa wa masuala ya jamii. Navyoelewa ni kwamba wasichana hawa wanataka kukuhusisha moja kwa moja katika hoja hii. |
| 96. | **TEACHER MONA** | Na mimi kama mwalimu, nasisitiza kwamba  Wasichana  lazima wahudhurie shule. Wakikosa kwenda shule ni kuwaharibia maisha yao. |
| 97. | **ELDER JACOB** | Nini kinachoendelea hapa? Kwani nimevamiwa…?.Ni rahisi sana kusema hivyo kwasababu mnacho chakula. Sisi hapa hatuna!!Lazima Fatuma afanye kazi! |

98. **JANET** Hilo ni jukumu la wazazi..kuzitimiza familia mahitaji yao yote na wala sio jukumu la mtoto.

99. **ELDER JACOB** Kwani huyu ni Mtoto?.

100. **JANET** Ilmradi bado yuko shuleni, yeye ni Mtoto.Mtoto ni jukumu lako.Kulingana na shirika la Umoja wa Mataifa linalowashughulikia watoto la UNICEF, watoto wengi katika Mataifa yaliyoko kusini mwa Jangwa la Sahara wanafanyishwa kazi. Na huu ni ukiukaji wa haki za watoto.

101. **ELDER JACOB** (ANGRY) Ukiukaji?! Sasa mmekuja kunishtaka?.. kwamba nakiuka haki za mtoto wangu?

102. **JANET** Hapana Mzee Jacob hatukuja hapa kukushtaki bali tuko hapa kuelimishana na tunayajali sana maslahi ya Fatuma. Kama nilivyosema, kulingana na sheria za shirika hili la UNICEF kuhusu haki za Watoto, unawajibu wa kulinda haki za Watoto hawa. Na hatua ya kumtoa Fatuma shuleni ili afanye kazi mchana kutwa,ni ukiukaji wa sheria hizi..!

| | | |
|---|---|---|
| 103. | **ELDER JACOB** | Sasa nimenza kuumwa na kichwa. |
| 104. | **TEACHER MONA** | Bado, kitakuuma sana pale Fatuma atakapokosa masomo, na kushindwa kujisaidia, na kukusaidia wewe na familia nzima katika siku zijazo. Mzee Jacob lazima uweke rasilimali zako katika elimu ya binti yako, ili uweze kunufaika siku zijazo.Hii ni rasilimali kubwa. |
| 105. | **ELDER JACOB** | (SHOCKED) Nini? Fatuma wangu? |
| 106. | **CIRO** | Mzee Jacob, tafadhali mwache Fatuma arudi shule. Ni rafiki yetu mkubwa na tumemkosa sana darasani. |
| 107. | **CHEPTOO** | Sawa…sawa… kimya kila mmoja. Je kuna Mtu kati yetu amewahi kumuuliza Fatuna anataka nini maishani? Fatuma,umenyamaza sana!. Hebu tueleze unataka nini? |
| 108. | **FATUMA** | (FIRMLY) Sitaki kufanya kazi.Kwani hivyo najihisi kuwa mimi ni punda.Nakata kuendelea na masomo yanguSitaki kuwa mjinga na kukosa kazi baadaye.(CRIES) |

| | | |
|---|---|---|
| 109. | **ELDER JACOB** | Samahani binti yangu, sikujua kwamba hayo ndio matakwa yako. |
| 110. | **TEACHER MONA** | Mzee Jacob, fikiria maisha ya baadaye ya Mtoto wako. Hebu tumpe nafasi afisa wa masuala ya jamii atueleze njia bora muafaka za kutafuta chakula familia yako. Fatuma hapasi kutumia kuitafutia familia hii chakula.Ni lazima tabia ya kuwafanyisha kazi watoto ikomeshwe mara moja. |
| **111.** | **JANET** | Niko tayari kukupa ushauri wakati wote. Lakini kwa sasa tunafunga mjadala huu kwa kusema '**Lazima tukomeshe ajira kwa watoto'** |
| 112. | **CHEPTOO** | Naunga mkono.Hakuna Mtoto yeyote anayepasa kuajiriwa.Fatuma sharti arudi shuleni. |
| 113. | **CIRO** | Mwalimu Mona, pia tunahitaji kuwatafuta wazazi wa watoto wanaozurura na kuuza njugu barabarani na hata shuleni mwetu. |
| 114. | **CHEPTOO** | (SLOWLY) Ni kweli.Singekuwa nanunua njugu zile. Ndio maana tumbo langu huchafuka kila mara. |

| | | |
|---|---|---|
| 115. | **TEACHER MONA** | Sawa tumekubaliana. Fatuna ni lazima arudi shuleni, na nyinyi wasichana mwende kuwatafuta wazazi wa watoto wanaouza Njugu. Lazima tukomeshe kabisa ajira kwa watoto.. |
| 116. | **ELDER JACOB** | (EXCITED) Sawa … sawa… eehh..ningependa kufanya mazungumzo na wazazi wa wasichana hao..endapo..endapo.. endapo…mtanipa nafasi |
| 117. | **CIRO/CHEPTOO/FATUMA** | Saaaaaawa….. (CLAPPING) |
| 118. | **JANET** | Sasa tunangoja nini, twendeni.Hatutaki ajira ya watoto!! |

119. **Outro**

120. **NARRATOR**

Na hadi hapo tunafika mwisho wa makala ya leo ya Noa Bongo Jenga maisha yako. Ungana nasi tena kwa makala nyingine ufahamu mengi kuhusu juhudi za wasichana hawa kufahamu haki zao. Endapo ungependa kukisikiliza tena kipindi hiki au kutuma maoni yako, tembelea mtandano wetu wa www.dw-world.de/lbe. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.